

DALILI ZA KIAKILI ZA KUMFAHAMU MWENYEEZI MUNGU

<"xml encoding="UTF-8?">

BISMILAHİ RAHMANİ RAHIYMI

DALILI ZA KIAKILI ZA KUMFAHAMU MWENYEEZI MUNGU

Katika makala zilizopita tulielezea njia za kumfahamu Mwenyeezi Mungu, na tukathibitisha .hayo kutokana na dalili za kiakili ambazo tulizithibitisha kutoka ndani ya Qur-ani

Katika makala hii tutaendelea kuziorodhesha Aya za Qur-ani ambazo kiakili zinathibitisha .kumfahamu na kumtambua Mwenyeezi Mungu

--:Mwenyeezi Mungu Mtukufu anasema

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَتَّخِذُوا بَطَانَةً مِّن دُونِكُمْ لَا يَأْلُونَكُمْ خَبَالًا وَدُّوا مَا عَنِتُّمْ قَدْ بَدَتِ الْبَغْضَاءُ مِنْ أَفْوَاهِهِمْ وَمَا تَخْفَى صُدُورُهُمْ أَكْبَرُ قَدْ بَيَّنَّا لَكُمُ الْآيَاتِ إِن كُنْتُمْ تَعْقِلُونَ[1]

Enyi mlio amini! Msiwafanye wasiri wenu watu wasio kuwa katika nyinyi. Hawataacha kukufanyieni ubaya. Wanayapenda yanayo kudhuruni. Imekwisha fichuka chuki yao katika midomo yao. Na yanayo ficha vifua vyao ni makubwa zaidi. Tumekwisha kubainishieni Ishara .ikiwa nyinyi mtayatia akilini

Maelezo kuhusiana na aya

Katika jambo kubwa kabisa linaloongoza mambo ya watu yakaongoka ni kuyapanga na kuyatengeneza kwa siri,yaonekane yamekwisha kusimama; kwani kuna waovu wengi, hawapendi ya wenzao yanyoke,basi mara huyatilia kila namna ya miunda; tahamaki .yamepwelewa papo hapo, hayawezi kwenda mbele

Ndio ikakatazwa hapa kuwafanya wasiokuwa Waislamu kuwa wasiri wenu wa kuwapa habari .zenu za ndani

Ama urafiki wa hujambo sijambo haukatazwi; wala kuwafanyia mema na insafu, kama .yalivyobainishwa haya katika aya ya nane ya Suratul-Mumtahina

لَا يَنْهَاكُمُ اللَّهُ عَنِ الَّذِينَ لَمْ يُقَاتِلُوكُمْ فِي الدِّينِ وَلَمْ يُخْرِجُوكُم مِّن دِيَارِكُمْ أَن تَبَرُّوهُمْ وَتُقْسِطُوا إِلَيْهِمْ إِنَّ اللَّهَ يُحِبُّ الْمُقْسِطِينَ[2]

Mwenyezi Mungu hakukatazini kuwafanyia wema na uadilifu wale ambao hawakukupigeni vita, wala hawakukutoeni makwenu. Hakika Mwenyezi Mungu huwapenda wafanyao uadilifu

Basi Mwenyezi Mungu hatukatazi kuwafanyia makafiri wema na insafu. Bali anatuamrisha .tuwafanyie haya

لَيْسَ عَلَيَّ الْأَعْمَىٰ حَرْجٌ وَلَا عَلَيَّ الْأَعْرَجُ حَرْجٌ وَلَا عَلَيَّ الْمَرِيضِ حَرْجٌ وَلَا عَلَيَّ أَنْفُسِكُمْ أَنْ تَأْكُلُوا مِنْ بُيُوتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ آبَائِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أُمَّهَاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ إِخْوَانِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أَخَوَاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أَعْمَامِكُمْ أَوْ بُيُوتِ عَمَّاتِكُمْ أَوْ بُيُوتِ أَخَوَالِكُمْ أَوْ بُيُوتِ خَالَاتِكُمْ أَوْ مَا مَلَكَتُمْ مَفَاتِحَهُ أَوْ صَدِيقَكُمْ لَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَنْ تَأْكُلُوا جَمِيعاً أَوْ أَشْتَاتاً فَإِذَا دَخَلْتُمْ بُيُوتاً فَسَلِّمُوا عَلَيَّ أَنْفُسِكُمْ تَحِيَّةً مِّنْ عِنْدِ اللَّهِ مُبَارَكَةً طَيِّبَةً كَذَلِكَ يُبَيِّنُ اللَّهُ لَكُمْ الْآيَاتِ لَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ [3]

Si vibaya kwa kipofu, wala si vibaya kwa kiguru, wala si vibaya kwa mgonjwa, wala kwenu nyinyi, mkila katika nyumba zenu, au nyumba za baba zenu, au nyumba za mama zenu, au nyumba za kaka zenu, au nyumba za dada zenu, au nyumba za ami zenu, au nyumba za shangazi zenu, au nyumba za wajomba zenu, au nyumba za dada wa mama zenu, au za mlio washikia funguo zao, au rafiki yenu. Si vibaya kwenu mkila pamoja au mbali mbali. Na mkiingia katika nyumba, toleaneni salamu, kuwa ni maamkio yanayo toka kwa Mwenyezi Mungu, yenye baraka na mema. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu anavyo kubainishieni Aya zake mpate .kuelewa

أَفْ لَّكُمْ وَلِمَا تَعْبُدُونَ مِنْ دُونِ اللَّهِ أَفَلَا تَعْقِلُونَ [4]

Aibu yenu nyinyi na hivyo mnavyo viabudu badala ya Mwenyezi Mungu! Basi nyinyi hamtii ?akilini

وَمَا أَوْتِيتُمْ مِّنْ شَيْءٍ فَمَتَاعُ الْحَيَاةِ الدُّنْيَا وَزِينَتُهَا وَمَا عِنْدَ اللَّهِ خَيْرٌ وَأَبْقَىٰ أَفَلَا تَعْقِلُونَ [5]

Na chochote mlichopewa ni matumizi ya maisha ya dunia na pambo lake. Na yaliyoko kwa .?Mwenyezi Mungu ndio bora na yatakayo baki zaidi. Basi je, hamfahamu

وَلَقَدْ أَصَلَّ مِنْكُمْ جِبِلًّا كَثِيرًا أَفَلَمْ تَكُونُوا تَعْقِلُونَ [6]

Na bila ya shaka yeye amekwisha lipoteza kundi kubwa miongoni mwenu. Je, hamkuwa ?mkifikiri

وَهُوَ الَّذِي يُحْيِي وَيُمِيتُ وَلَهُ اخْتِلَافُ اللَّيْلِ وَالنَّهَارِ أَفَلَا تَعْقِلُونَ [7]

Na Yeye ndiye anaye huisha na kufisha, na yake Yeye mabadiliko ya usiku na mchana. Basi je!

هُوَ الَّذِي خَلَقَكُمْ مِّن تَرَابٍ ثُمَّ مِّن تُّفْفَةٍ ثُمَّ مِّن عَلَقَةٍ ثُمَّ يُخْرِجُكُمْ طِفْلاً ثُمَّ لِيَبْلُغُوا أَشَدَّكُمْ ثُمَّ لِيَتَّكُونُوا شُيُوخاً وَمِنْكُمْ مَّن يُّتَوَفَّى مِن قَبْلٍ وَلِيَبْلُغُوا أَجْلاً مُّسَمًّى وَلَعَلَّكُمْ تَعْقِلُونَ[8]

Yeye ndiye aliye kuumbeni kwa udongo, kisha kwa tone la manii, kisha kwa pande la damu, kisha akakutoeni katika hali ya mtoto mchanga, kisha mpate kufikilia utu uzima, kisha mpate kuwa wazee. Na kati yenu wapo wanao kufa kabla, na ili mfikie muda ulio kwisha wekwa, na ili .mpate kufahamu

وَبِاللَّيْلِ أَفْلاً تَعْقِلُونَ[9]

?Na usiku. Basi je! Hamyatii akilini

فَخَلَفَ مِنْ بَعْدِهِمْ خَلْفٌ وَرِثُوا الْكِتَابَ يَأْخُذُونَ عَرَضَ هَذَا الَّذِي يُقُولُونَ سَيُعَذِّبُنَا وَإِن يَأْتِهِمْ عَرَضٌ مِّثْلَهُ يَأْخُذُوهُ أَلَمْ يُؤْخَذْ عَلَيْهِمْ مِّيثَاقُ الْكِتَابِ أَن لَّا يَقُولُوا عَلَى اللَّهِ إِلَّا الْحَقَّ وَدَرَسُوا مَا فِيهِ وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ لِلَّذِينَ يَتَّقُونَ أَفَلَا تَعْقِلُونَ[10]

Na wakafuatia baada yao kizazi kibaya walio rithi Kitabu. Wakashika anasa za haya maisha duni, na wakasema: Tutasamehewa! Na ikiwajia tena anasa kama hiyo wataishika pia. Je, hawakufanyiwa agano la Kitabu kuwa wasiseme juu ya Mwenyezi Mungu ila Haki tu? Nao wamekwisha soma yaliomo humo. Na nyumba ya Akhera ni bora kwa wanao jikinga na maasi.

Basi je, hamtii akilini? .

Maelezo kuhusiana na aya

Sifa hii ya Mayahudi wabaya ya kufanya uovu bila ya kujali kwa kutaraji kusamehewa juu ya ubaya wao huo; sifa hiyo imerithiwa na baadhi ya Waislamu sasa. Kuna chungu ya Waislamu- na wengineo katika wao ni wajuzi wa dini- wanaodhulumu huku na kufisidi huku, wakiambiwa wanasema: “Mwenyeenzi Mungu Ghafur” uwongo maneno haya; na Mwenyeenzi Mungu anayakataa hapa aliyoyakataa mahala pengi kabisa penginepo kama katika aya ya 17 na 18 .suratul-Nisaa. Na Mtume pia amekanusha habari hii

إِنَّمَا التَّوْبَةُ عَلَى اللَّهِ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ الشُّوَاءَ بِجَهَالَةٍ ثُمَّ يَتُوبُونَ مِن قَرِيبٍ فَأُولَٰئِكَ يَتُوبُ اللَّهُ عَلَيْهِمْ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيماً حَكِيماً

وَلَيْسَتِ التَّوْبَةُ لِلَّذِينَ يَعْمَلُونَ السَّيِّئَاتِ حَتَّىٰ إِذَا حَضَرَ أَحَدَهُمُ الْمَوْتُ قَالَ إِنِّي تُبْتُ الْآنَ وَلَا الَّذِينَ يَمُوتُونَ وَهُمْ كُفَّارٌ أُولَٰئِكَ أَعْتَدْنَا لَهُمْ عَذَاباً أَلِيماً[11]

Hakika toba inayo kubaliwa na Mwenyezi Mungu ni ya wale wafanyao uovu kwa ujinga, kisha

wakatubia kwa haraka. Hao ndio Mwenyezi Mungu huwakubalia toba yao, na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi na ni Mwenye hikima .Wala hawana toba wale wafanyao maovu mpaka yakamfikia mmoja wao mauti, kisha hapo akasema: Hakika mimi sasa nimetubia. Wala wale wanao kufa .na hali wao ni makafiri. Hao tumewaandalia adhabu chungu

Hii ni itikadi mbaya tuliyowafuata Mayahudi. Na kuna mengineyo pia tuliowafuata Mayahudi na .Manasara na wenye dini nyenginezo

Na Mtume alitwambia haya kuwa tutapotea baadhi yetu; tutafuata itikadi na nyendo za watu wenye dini nyengine tuache itikadi za dini yetu na njia yake iliyonyooka, alisema haya Mtume Kwa lafdhi hizi: “ Mtafuata nyendo za wale waliokuwa kabla yenu. Mtawafuata shubiri kwa shubiri. Hata lau wangeingia katika shimo la kenge basi na nyinyi mtaingia” Kama mambo haya ya kujitumainisha uwongo, mambo ya kukumbusha misiba na kuacha yaliyo muhimu wakashughulikia ya upuzi.

Na kila aya zilizowateremkia makafiri basi na wabaya hawa wanaowafuata zinawachukua. Husemwa hivi ndani ya vitabu, husemwa” Kila aya iliyowateremkia makafiri basi huwakokota .na maasi wa kiislamu.” Basi natutahadhari na kutupa mwendo wetu na itikadi zetu za Kiislamu

Kutokana na aya hizo tulizoziorodhesha hapo juu inathibitisha ya kwamba qur-ani kariym inawaamrisha watu kuzingatia na kufikiri, hii ni kwa sababu ya dalili ambazo zinamuongoza mwanaadamu katika njia ya Mwenyeenzi Mungu mtukufu. Katika sehemu hii tutaashiria baadhi .ya dalili na kutoa mifano yake

Surat Al-im-rani aya ya 118 [1]

Suratul-mumtahina aya ya 8 [2]

Surat Nuur aya ya 61 [3]

Surat Anbiyaa aya ya 67 [4]

Suratul-Qasas aya ya 60 [5]

Surat Yaasin aya ya 62 [6]

Suratul-Muu-minuun aya ya 80 [7]

Surat Ghaafir aya ya 67 [8]

Surat Ghaafir aya ya 138 [9]

Suratul-Al-aaraf aya ya 169 [10]

Suratul-nisaa aya ya 17-18 [11]

MWISHO